

Katika dunia ya sasa inayosongwa na changamoto za mahusiano , kutafuta na kuanzisha mahusiano ya kudumu yenyе msingi wa upendo wa kweli na heshima imekuwa safari yenyе changamoto kubwa kwa wanawake wengi.

Wanawake wengi wamejikuta wakifanya maamuzi yanayoathiri maisha yao kwa sababu ya ukosefu wa mwongozo sahihi wa kumsaidia kuelewa ni nini haswa kinachohitajika ili kuanzisha na kujenga mahusiano yenyе afya.

Baada ya tafakari ya hayo yote ndipo wazo la kuandika hiki kitabu lilipozaliwa.

Kitabu hiki ni muongozo wa kukusaidia mwanamke kuelewa thamani yako ili umpate mwanaume wa hadhi yako, mchakato wa kumpata mwanaume umtakaye kwa mbinu ya mvuto.

Lakini si hayo tu utakayo jifunza kwenye hiki kitabu bali utajifunza pia namna ya kujipenda na kujipa thamani kitu ambacho ni msingi wa mahusiano yote ya mapenzi.

Aidha, kitabu hiki kimeeleza kwa kina jinsi ya kuishi maisha ambayo si tu yanakufanya uonekane mwenye thamani, bali pia yanakufanya ustawi katika nyanja zote za maisha yako.

Utajifunza jinsi ya kujiboresha kimwili, kiakiri na kiroho, na hivyo kujenga haiba ya kuvutia na inayodhihirisha ujasiri na nguvu za ndani.

Kwa kufuata mafunzo ya kitabu hiki, utajikuta ukiwa katika nafasi ya kipekee ya kuvutia mwanaume anayekuheshimu, anayekupenda, anayekubaliana na kuendana na kile ulichonacho ndani yako.

Kitabu hiki si tu mwongozo wa kumpata mwanaume sahihi bali pia ni mwaliko wa

kujiboresha na kuishi maisha ya thamani  
kama mwanamke.

Karibu uingie kwenye safari hii ya kubadili  
maisha yako.

Mimi ni ANJELA E.M.